

KANISA ANGLIKANA TANZANIA
CHUO CHA THEOLOJIA CHA MTAKATIFU FILIPO

TARATIBU YA IBADA
YA KUMUAGA BIBI HARUSI
MTARAJIWA




“Wakamwita Rebeka wakamwuliza, Je! Utakwenda na mtu huyu?
Akasema, Nitakwenda... Wakambarikia Rebeka, wakamwambia,
Ndugu yetu, uwe wewe mama wa kumi elfu, mara elfu nyingi.”
(Mwanzo 24:58, 60).

KANISA ANGLIKANA TANZANIA CHUO CHA THEOLOJIA CHA MT. FILIPO

TARATIBU YA IBADA YA KUMUAGA BIBI HARUSI MTARAJIWA

Kimetayarishwa na:

Rev Can Capt Agripa Ndatila – Mwalimu wa Ibada




St Philip's Theological College

Hakimiliki © St Philip's Theological College 2019

Toleo la Kwanza Septemba 07, 2019

Haki zote zimehifadhiwa.

Kimetolewa na kuchapwa na St Philip's Theological
College, S.L.P 26 Kongwa, Tanzania



TARATIBU YA IBADA YA KUMUAGA BIBI HARUSI MTARAJIWA

**Ibada hii ina sehemu kuu tatu: Ibada ya Neno, Ibada ya kumuaga Bibi Harusi mtarajiwa na Ibada ya ushirika mtakatifu (kama ipo).*

1. WIMBO WA KUANZA IBADA

2. UTANGULIZI

Mhudumu:

Ndugu wapendwa tumekusanyika hapa ili kumuaga binti yetu ambaye anatarajiwa kuolewa na wa ukoo wa

Tukumbuke kwamba wakati wa kumuaga bibi arusi ni wakati wa furaha kwa vile ni hatua muhimu kabla ya kufunga ndoa.

Niwakaribisheni nyote tuungane pamoja kumshukuru Mungu kwa binti yetu huyu, tumwombee anapojiandaa kufunga ndoa na kuanza kuishi na mume wake mtarajiwa; na tumtakie heri katika maisha mapya ya anayotarajia kuyaanza.

Tuianze ibada hii kwa jina la Baba na mwana na Roho Mtakatifu.

Watu: **Amin.**

3. *Mhudumu aseme Amri Kuu au Amri Kumi*

Bwana wetu Yesu Kristo alisema. Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa akili zako

zote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii.

Au Amri Kumi:

Mungu akanena maneno haya yote akasema:
Mimi ni Bwana Mungu wako,
Usiwe na miungu mingine ila mimi.
Usijifanyie sanamu ya kuchonga ukaiabudu.
Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako.
Ikumbuke siku ya Bwana, uitakase, siku sita fanya kazi.
Uwaheshimu baba yako na mama yako.
Usiue.
Usizini.
Usiibe.
Usimshuhudie jirani yako uongo.
Usitamani kitu chochote alichonacho jirani yako.

4. *Kisha isemwe Bwana Uturehemu*

Bwana uturehemu

Bwana uturehemu

Kristo uturehemu

Kristo uturehemu

Bwana uturehemu

Bwana uturehemu

Msaada wetu ni katika jina la Bwana

Aliyeziumba mbingu na nchi

Mhudumu:

Wapendwa katika Bwana, tumuungamie Mungu dhambi zetu, kwa moyo mnyenyekevu, uliotubu na kutii; ili tupate kusamehewa kwa wema na rehema zake zisizo na kikomo.

5. *Ungamo:*

Mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni, twaungama kwamba tumekutenda dhambi wewe na jirani zetu; kwa mawazo na maneno na matendo, na kwa kutokutimiza yatupasayo. Twasikitika sana, twatubu, kwa njia ya Yesu Kristo utusamehe na kutusafisha kwa Roho wako Mtakatifu; ili tuweze kukutumikia katika upya wa maisha, kwa utukufu wa jina lako. **Amin.**

6. *Kasisi asimame na atoe ghofira:*

Mwenyezi Mungu anayewasamehe wote watubuo kwa kweli, akurehemuni, akusameheni dhambi zenu zote, akutieni nguvu, akuimarisheni katika wema wote; akufikisheni kwenye uzima wa milele; kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Watu: **Amin**

7. *Watu wakiwa wamesimama waseme au kuimba Utukufu:*

Utukufu una Mungu juu Mbinguni:

Amani duniani kwa watu aliowaridhia.

Twakusifu, Twakuhimidi

Twakuabudu,

Twakutukuza,

Twakushukuru,

Kwa ajili ya utukufu wako mkuu.

Bwana Mungu,
Mfalme wa mbinguni,
Mungu Baba mwenyezi.
Ee Bwana, Mwana pekee, Yesu Kristo, Bwana Mungu,
Mwana kondoo wa Mungu,
Mwana wa Baba; Uichukuaye dhambi ya ulimwengu,
Uturehemu;
Uichukuaye dhambi ya ulimwengu,
Ukubali kuomba kwetu;
Uketie mkono wa kuume wa Mungu Baba,
Uturehemu.
Kwa kuwa ndiwe peke yako Mtakatifu,
ndiwe peke yako Bwana,
ndiwe peke yako uliye juu,
Yesu Kristo,
Pamoja na Roho Mtakatifu,
Katika utukufu wa Mungu Baba.
Amen.

Mhudumu: Bwana akae nanyi
Watu: **Pia na Roho yako**

Mhudumu: Tuombe

8. SALA YA SIKU

9. HUDUMA YA NENO

10. SOMO: MWANZO 24: 47 - 61

11. WIMBO:

12. MAHUBIRI:

13. IBADA YA KUMUAGA BIBI HARUSI MTARAJIWA

WIMBO WA KUMLETA BIBI HARUSI MTARAJIWA

****Wakati wimbo unaimbwa, Bibi Harusi mtarajiwa na Mpambe wake wataletwa na kaka yao/zao katika viti vilivyo katikati ya kanisa wakiketi kuwaelekea watu.***

HISTORIA YA BIBI HARUSI:

****Historia ya Bibi Harusi mtarajiwa, itasomwa na kaka waliomleta ikielezea maisha yake tangu kuzaliwa hadi sasa kwa kutaja mafanikio, changamoto, matamania na mapendeleo.***

****Maneno ya Ukaribisho kwa familia ya Bwana Harusi Mtarajiwa:***

Kaka:

Sisi kaka wa Bibi Harusi mtarajiwa, kama ilivyokuwa kwa mwana wa Bethueli na Nahori aitwaye Labani, aliposikia habari ya mtumwa wa Ibrahimu aliyekuja kumposea mwana wa Bwana wake mke; alimwendea kisimani kumlaki na kumkaribisha nyumbani kwa ajili ya taratibu za kuolewa kwa dada yao. Mtumishi aliapa kuwa hali chakula mpaka atakapofikisha ujumbe wa kumposea mwana wa Bwana wake mke. Kwa sababu hiyo basi, sisi kama kaka wa mtarajiwa tunaomba kama kuna ndugu yeyote wa Bwana Harusi mtarajiwa, ajitokeze ili atuambie ametumwa na ukoo wa nani kuja kumposea mwanawe dada yetu, na atuambie huyo mwana anaitwa nani, na ana uthibitisho gani wa kutumwa na ukoo wa Bwana wake.

****Mjumbe wa Bwana Harusi mtarajiwa aje mbele ya kaka wa bibi Harusi mtarajiwa na kuitika mwito kwa kusema:***

Mjumbe: Salaam kaka za Bibi Harusi Mtarajiwa

Kaka: Salaam Mjumbe

****Bibi Harusi mtarajiwa apige magoti mbele ya mjumbe na kusema:***

Bibi Harusi Mtarajiwa:

Pole kwa safari ndefu, karibu kwetu.

Mjumbe: Asante, namshukuru Mungu nimefika salama.

Bibi Harusi mtarajiwa:

Pokea maji unywe, upoze kiu baada ya safari ndefu.

****Mjumbe apokee na kunywa maji kama Rabeka alivyofanya ukaribu kwa mjumbe na Ibarahimu, na kisha aseme:***

Mjumbe:

Mimi..... niliyetumwa na
kumposea mke kijana wake aitwaye
Nasimama mbele yenu na mbele ya Mungu nikithibitisha
kwamba, kijana wetu amedhamilia kwa dhati
kumuoa dada yenu aitwaye Kwa sababu
hiyo basi ninawaomba mnifungulie kiapo changu kwa
kunipatia msichana huyo ili aolewe na kijana wa Bwana
wangu. Kwa upendo tulio nao, tunakuomba Bibi Harusi
wetu mtarajiwa, kaka, na wazazi mpokee zawadi
tulizoleta kwenu kama ishara ya upendo wetu.

Kaka: Tumepokea kwa shukurani. Lakini kwanza tunaomba tupate ridhaa ya dada yetu.

**Ndipo wageuke aliko Dada yao na kusema:*

Kaka:

Dada yetu, umesikia maneno aliyosema mjumbe wa kusema kuwa amekuja kumposea mwanawe mke, naye amekuona wewe. Tunakuuliza basi: “Je! Utakwenda na mtu huyu na uko tayari kuolewa na mwana wa Bwana wake?”

Bibi Harusi mtarajiwa: Niko tayari, nitakwenda.

Watu wote: **Wapige makofi, vigelegele na kushangilia.**

**Mjumbe wa familia ya Bwana Harusi arudi kwenye kiti na ndipo kaka za Bibi Harusi waende kwa wazazi wao na kuwaleta kwa ajili ya maneno ya kwaheri na wosia kwa Bibi Harusi mtarajiwa.*

Kaka: “Ndugu yetu, uwe wewe mama wa kumi elfu mara elfu nyingi na wazao wako waurithi mlango wa hao wawachukiao” (mwanzo.24:58-60).

Kaka: Na sasa dada yetu kama tulivyolelewa vizuri na wazazi wetu wakatuusia maneno mengi ya msingi, leo wako mbele yako kukuaga na kukupa wosia. Karibu wazazi wetu kwa kumpa dada yetu mbaraka wenu.

**Maneno ya kwaheri na wosia toka kwa Wazazi wa Bibi Harusi Mtarajiwa yatolewa kwa kadri walivyojipanga.*

14. SALA ZA KUMWOMBEA BIBI HARUSI MTARAJIWA

**Bibi Harusi mtarajiwa na mpambe wapige magoti kuelekea madhabahuni*

Mhudumu	Tuombe
Mhudumu:	Ee Mungu uwe radhi kutuokoa
Watu:	Ee Bwana utusaidie hima
Mhudumu:	Msaada wetu ni Katika Jina Bwana
Watu	Aliyeziumba mbingu na nchi

Mhudumu:

Ee Mungu wa Ibrahimu na sara, Mungu wa Zakaria na Elizabeth, Mungu wa Yusufu na Mariamu. Tangu mwanzo ulitaka mtu mume aishi na mtu mke na ukawabariki ili waweze kuijenga familia. Tunakuomba umjalie msichana huyu maisha mema na kumjalia maisha ya kudumu akiwa mke mwema hata mwisho aupate uzima wa milele; kwa Yesu Kristo Bwana Wetu. **Amen.**

**Kasisi amnyunyizie maji ya Baraka au kuchora alama ya msalaba, na kisha amshike mkono wa kulia na kumbariki kwa kusema:*

Mhudumu:

Mungu akuangazie nuru ya uso wake na kukufunika, † akulinde na hatari na mabaya yote, † akufikishe salama siku ya Ndoa yako ukiwa na afya na uzima tele, † ambariki mume wako mtarajiwa ili afanyike Baraka kwako, † Aijalie nyumba yako Baraka na Amani, † kwa Yesu Kristo Bwana Wetu. **Amen.**

****Sala ya kumwombea Bibi Harusi na Mume mtarajiwa:***

Mhudumu:

Mungu wa upendo tunakushukuru kwa kumjalia binti huyu kutunza maisha yake hadi kufikia siku hii ya familia yake kumuaga kwa furaha, ili baada ya kufunga ndoa akaishi na mumewe. Tunakushukuru hata kwa kumpatia mume mtarajiwa ambaye anampenda na tunaamini kwamba ataishi nae kwa furaha. Twakuomba uwajalie afya, upendo na mshikamano wa kweli hata waifikie siku hiyo ambayo sote tunaitazamia. Twaomba haya kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu **Amin.**

****Sala ya kuwaombea wazazi wa maarusi wataraji:***

Mhudumu:

Baba Mwenyezi na mwenye rehema, tunakushukuru kwa wazazi wa Bibi harusi, walio mlea vizuri binti yao hadi kufikia hatua hii ambayo ameifikia. Twakuomba uwajalie afya njema wao pamoja na wazazi wa bwana harusi mtarajiwa hadi waifikie siku ile ambayo furaha yao itakamilika. Wajalie upendo, amani na ushirikiano wanapofanya maandalizi ya vijana wao hawa. Kwa Yesu kristo Bwana wetu. **Amin.**

Mhudumu:

Sala ya kuombea maandalizi ya ndoa.

Tuombe:

Mwenyezi Mungu Baba wa mbinguni, tunakuja mbele zako tukikuomba utangulie na kuzibariki shughuli zote za maandalizi ya ibada ya ndoa na sherehe ya watoto wako hawa na.....Tunakuomba ubariki mipango ya ibada ya kukamilisha ndoa yao itakayofanyika siku chache zijazo. Tunakuomba uwajalie maisha mema yaliyojengwa katika mafundisho na Imani ya Kikristo, na tunakuomba wasimame imara katika upendo na ukarimu katika nyumba yao. Twaomba haya Eee Bwana tukiamini kwamba utajibu maombi yetu haya kwa jinsi tulivyokuomba; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amin.**

Sala ya Bwana:

**Baba yetu uliye mbinguni, jina lako
litukuzwe.....**

- 15. WIMBO WA SADAKA
- 16. SALA YA KUOMBEA SADAKA
- 17. MATANGAZO/UTAMBULISHO
- 18. BARAKA

****Endapo kama ibada haitakuwa na ushirika Baraka itolewe
baada ya ushirika mtakatifu)***

- 19. IBADA YA USHIRIKA MTAKATIFU IENDELEE KAMA
ILIVYO KATIKA KITABU CHA SALA.

****Ndipo shamrashamra nyingine za zawadi, pongezi, chakula na kama kuna
taratibu zingine kama vile salam mbalimbali zifuate kabla ya Baraka ya
mwisho.***

- 20. WIMBO WA KUTOKA